



### Mji wa Boise

**Mpango wa 2022 wa virusi vya corana wa ruzuku ya kurejesha fedha**

**Kiambatisho C: Vigezo vya kustahiki na vipaumbele**

**Nyongeza: Uainishaji wa kanuni za NAICS**

Kagua orodha ya tasnia za biashara zilizohitimu na maelezo yake kwa uangalifu. Je, biashara yako ni mojawapo ya sekta zifuatozo zilizohitimu? Kama ndio, tafadhalii kumbuka kanuni ya NAICS (North American Industry Classification System) kwenye ombi ya ruzuku ya biashara ndogo ya mji wa Boise.

**3283 – Wakandarasi wa Ujenzi na kumaliza majengo Wakandarasi wa Kumaliza Majengo:**

Kikundi hiki cha tasnia kinajumuisha mashirika ambayo kimsingi yanashughulisha biashara maalum zinazo hitajika kumaliza majengo. Kazi inaweza kujumuisha kazi mpya, nyongeza, mabadiliko, matengenezo, na ukarabati.

**44-45 – Biashara za Rejareja:** Kikundi hiki cha tasnia kinajumuisha mashirika yanayojishughulisha na uuzaji wa rejareja, kama vile masoko ya nguo na chakula, ambayo kwa kawaida huuzia umma bidhaa za matumizi ya kibinagsi au ya nyumbani.

**6216 – Huduma za Afya ya Nyumbani:** Kukundi hiki cha tasnia kinajumuisha taasisi zinazo jishugulisha na kutoa huduma za uuguzi wenyewe ujuzi nyumbani pamoa na anuwai ya huduma zifuatazo; utunzaji wa kibinagsi; wahudumu wa nyumbani na wenzi; tiba ya mwili; huduma za matibabu za kijamii; madawa; vifaa vya matibabu; na ushauri.

**72 – Huduma za Malazi na Chakula:** Kikundi hiki cha tasnia hii kinajumuisha uanzishaji unoajishughulisha na kuwapa wateja malazi na/au kuandaa milo, vitafunio na vinywaji kwa matumizi ya haraka.

**71 – Sanaa, Matumbuizo na Burudani:** Kikundi hiki cha tasnia kinajumuisha taasisi zinazosimamia majengo au kutoa huduma ili kukidhi matakwa tofauti ya kitamaduni, matumbuizo na burudani kwa wateja wao.

**811 – Ukarabati na Matengenezo:** Viwanda katika sekta ya ukarabati na matengenezo hurejesha mashine, vifaa, na bidhaa zingine katika hali ya kufanya kazi. Taasisi hizi pia hutoa matengenezo ya jumla au kawaida, sawa na ukaguzi wa kawaida, kwenye vifaa hivyo ili kuhakikisha vinafanya kazi kwa ufanisi kuzuia kuharibika na matengenezo yasiyo ya lazima.

**8111 – Ukarabati na Matengenezo ya Magari:** Kikundi hiki cha tasnia kinajumuisha mashirika ambayo yanahusikana na ukarabati na utengenezaji wa magari, kama vile magari ya abiria, lori, na trela.

**8112 – Urekebishaji wa vifaa vya Elektoniki na Usahihi:** Kikundi hiki cha tasnia kinajumuisha taasisi za ukarabati na matengenezo ya vifaa vya elektroniki, komputa za ofisini na mashine, vifaa vya matibabu, na mawasiliano.

**8114 – Ukarabati wa Bidhaa za Kibinafsi na za Nyumbani:** Kikundi hiki cha tasnia kinajumuisha taasisi zinazojishughulisha kimsingi na vifaa vya nyumbani na bustani na ukarabati na matengenezo ya vifaa; ukarabati wa samani; ukarabati wa viatu na bidhaa za ngozi; na ukarabati wa bidha zingine za kibinafsi na za nyumbani.

**81211 – Huduma za Utunzaji wa Nywele, Kucha na Ngozi:** Kikundi hiki cha tasnia kinajumuisha taasisi inayotoa huduma za utunzaji wa nywele; utunzaji wa kucha; utaalamu wa kunyosha/kukanda mwili; za usoni au kupaka vipodozi (isipokuwa vipodozi vya kudumu).

**812111 – Vinyozi:** Kikundi hiki cha tasnia kinajumuisha taasisi zinazojulikana kama duka za vinyozi wa nywele za wanaume ambao kimsingi hujishughulisha na kukata, kunyoa na kutia mitindo kwenye nywele za wanaume na wavulana; au kukata na kunyoa ndevu za wanaume.

**812112 – Saluni za Urembo:** kundi hili la tasnia linajumuisha mashirika ambayo hutoa moja au zaidi ya yafuatayo: kukata, kunyoa, kuosha nywele, kupaka rangi, kusuka au ketengeneza mtindo wa nywele, utunzaji wa uso, na kupaka vipodozi (isipokua vipodozi vya kudumu).

**812113 – Saluni za Kucha:** Kikundi hiki cha tasnia kinajumuisha taasisi zinazota utunzaji wa kucha, kama vile kutengeneza kucha za mikono, kucha za miguu na kubandika kucha bandia.

**812910 – Huduma za Wanyama (Isipokuwa mifugo):** Sekta hii inajumuisha taasisi inayojishughulisha na huduma za utunzaji wa wanyama kipenzi, (isipokuwa mifugo), kama vile bweni, mapambo, kukaa na mafunzo ya kipenzi.